**Jiwe La Kiroho Kujengea Na: 19**

# MUNGU HUPONYA

***Kutoka 15:26 "… Kwakua Mimi ndimi Bwana nikuponye"***

Wakati tunasikiliza hizi nyimbo mzuri-Ndugu Branham anaongea na kusanyiko Phoenix-Nilizungumza na ndugu Outlaw " Ninafuraha zimerekodiwa,kwa sababu ninapenda kujifunza hizo. Ninapenda kusikia hizo nyimbo na kuchezea tu mkanda,sikiliza nyimbo na kucheza tu mkanda, sikiliza nyimbo wakati unaweza kukaa chini".

Hakuna kitu kama mziki unajua, Mungu huponya kwa mziki. Unalifahamu hilo? Mungu huponya kwa mziki (Nyimbo)

Mungu huponya kwa upendo. Unaona? Mungu huponya kwa dawa. Mungu huponya kwa maombi. Mungu ananjia nyingi za kuponya,hutegemea na aina gani unataka.

Wakati mwingine upendo mdogo, uliotengwa,utaponya tu ugonjwa wa muda mrefu, mahali pa-zamani ambapo pamechukiza au kitu fulani. Utaponya hicho , upendo kidogo tu,huduma kidogo tu.

Wakati mwingine wakati unapohisi yote chini na kama tu tunavyojiita hilo, chini ndani ya dampo, unaona, weka tu moja ya hizo kanda,hizo nyimbo aina ni kodi na nenda kuzicheze hizo.Kitu cha kwanza unajua utachezesha mguu wako au mkono wako na halafu yote yamekwisha, Unasimama na tayari kwa kuendeleza tena [1]

Sasa Mungu huponya kwa namna nyingi ***(1 Petro 2:24-25)*** Daktari aliniuliza , sio muda mrefu uliopita kusema, " Nikasema vema , Mungu ndio pekee anayeweza kuponya, Bwana " Nikasema Biblia haidanganyi, na biblia ilisema , " Mimi ni Bwana nikuponyae na Magonjwa yako yote. " ***(Zaburi 103:1-3)*** . Na nikasema " Biblia haiwezi kudanganya, Mungu huponya kwa dawa, Mungu huponya kwa maombi. Mungu huponya kwa miujiza. Kitu chote, Mungu huponya. Hiyo yote ni yote yako katika hilo, Yeye ni mponyaji.

Hatujapata dawa inayoweza kuumba na kuumba seli katika mkono wako, Kuponya kuumba ndani ya mwili wako, kuponya. Tunaweza kusogeza (kutoa) jino,tunaweza kutoa kidole tumbo, au kutoa kibofu lakini nani aliyeponya? Mungu hakuna dawa itakayo unda tishu, Mungu pekee. Uhai huunda tishu. Mungu ndiye mponye pekee, na tulikua tukizungumza kuhusu hilo. [2]

Ninamatumaini kwamba kila mmoja wenu amelipata hilo, (zaidi) ninyi watu mnavoenda kuombewa , hilo liko na wasiwasi zaidi kama labda shida ambayo daktari hawezi kugusa.

Natumaini daktari husaidia watu. Ninaamini kwamba huponya kwa dawa. Mungu huponya kwa upasuaji. Mungu huponya kwa ufahamu. Mungu huponya kwa upendo na Mungu huponya kwa maombi, Mungu huponya kwa upendo. Upendo mdogo unaenda njia ndefu (pa kubwa). Hebu watu fulani wawe wamekasirika, uoneshe tu wao unawajali, Unaona? Mungu huponya kwa upendo kwa upendo, Mungu huponya kwa maombi, Mungu huponya kwa miujiza, Mungu huponya kwa neno lake ***(Zaburi 107:20)*** Mungu huponya! Haijalishi chanzo ni kipi, Mungu huponya kwa hicho. Ni Mungu ndiye anaye, kwa maana amesema, “ Mimi ni Bwana ambaye huponya magonjwa hayo yote, “ kwa maana amesema, “ Mimi ni Bwana ambaye huponya magonjwa hayo yote” kwa hivyo hivyo vyote lazima vifanye kazi kwa na mwanadamu katika huduma tofauti lazima vifanye kazi pamoja kwaajili ya hilo. Unaona? Sasa , lakini hawafanyi hilo kwababu wakati mwingine wana uhalali kuchukua msimamo fulani juu ya neno la Mugu , kwa sababu dhehebu lao fulani haliwaruhusu wao kufanya hilo. Lakini hiyo haizuii ukweli ni vilevile tu, Mungu anaendekeza kuponya vilevile. [3]

“ Tumeona mtu ambaye anaweza kumuita mtu aliyekufa kutoka kaburini, Ambaye anaweza kufanya miujiza hii yote ya ajabu, na tunamuona yeye msalabani na mate negi usoni mwake mwote, na askari wakichezea ndevu zake, na mate usoni mwake mwote, na askari wakichezea ndevu zake na mate usoni pake. Nakumuona yeye mwongoni kwake amepigwa kwa mijeledi ambayo hupigwa kwa punda mistari thelathini na nane duniani leo. Michirizi thelathini na nane kwenye mgongo wake pamoja nap aka wa mikia tisa, tundu la ngozi ndani yake na uvimbe wa risasi,walimpiga mpaka mbavu zake zilionyesha, “ Mifupa yangu yote inanitzama mimi”, Alisema katika ***(Zaburi 22:9-17).*** (4)

Wakati tunapomuona Mungu akiponya mtu…Hapa muda mchache uliopita katika Kanisa letu,walimleta msichana mdogo katika machela, na walinita mimi wakati wa usiku barabarani na kusema “ Msichana hawezi kuishi” Kanisa ilikua ni mbaya

sana. Kama umri wa miaka kumi na saba “ Yeye hawezi hata kufika pale, angeenda kufa kabla hajafika pale” ilikuwa ni jambo lenye kusikitisha, mpendwa mtoto mdogo wa miaka kumi na saba.

Kuthibitisha kitu fulani kwa Kanisa langu, kamwe mimi sikumgusa kabisa yule mtoto. Nilitembea. Amelala kwenye machela “ kwa sababu kulikua na wagonjwa wengine , lakini nilihusika sana na mtoto,kukamata roho yake wakati ninazungumza naye na alionekana kama binti mzuri mdogo. Nikaona hakuna sababu kwanini yule mtoto mdogo kujaza (kuzikwa) kwenye kaburi la watoto; na huyo angekua ni shetani akijaribu kuchukua uhai kwahiyo sikumgusa kabisa mtoto, nikaenda mimbarani na neno, nikasimama na neno. Na neno likamponya yeye papo hapo mpaka akanyanyuka na kutembea ni yote sasa , anaishi kama mtu mwingine huwezi kupata maelezo ya hicho popote pale. Kamwe hata sikumgusa Yeye.

Unaona , neno linakwenda nje, na aliniamini neno, na Neno ni maisha ya Mungu na nguvu na nguvu ya Mungu. Na neno huwa kile lolote neno huponya mgonjwa ***(Marko 7:24-30; Mathayo 8:5-13)*** [5]

Usiku mwingine, ulikua wa kustajabisha sana. Msichana mdogo alikuja hapa jukwaani, ile dola miatatu elfu ameweka pale na alikua na shedo kidogo usoni pake. Alisimama pale na kuanza kutetemeka. Nikasema “ wewe ni mlutheri” Kwa Roho Mtakatifu. Yeye akasema , “ Ndio Bwana”. Na nikasema, “ Uko hapa kwaajili ya kombewa. Na sababu unatembea injili hiyo uliyo magoti yote yamevunjika, Nikasema , “ Hiyo ilisababishwa ajali ya gari katika gari uliokua unaendesha miaka minne iliyopita” Akasema “Hiyo ni kweli” Nikasema “ Daktari wako mfupi hivi mwenye upaa na anavaa miwani” Akasema “ Hiyo ni sawa” Nikasema “ Udaktari wake, kwasababu pale ndani ya magoti mfupa umekua nundu na pia nyama imeoza kuzunguka mfupa” Akasema hiyo ni kweli”.

Akasema “kuna tumaini kwaajili yangu”? Nikasema “ hapana maana. Hakuna anayeweza kukusaidia sasa, lakini anapaswa kujisaidia mwenyewe kwa Baraka zilizoandaliwa na Mungu kwaajili yako” Na akasema “ Ninaaminji sasa kwa moyo wangu wote” Nikasema “ Mungu amekuponya, dada ni HII ASEMA BWANA , Umeponywa”.

Akasema “ Bwana Branham, sikua na uwezo wakukunja goti” Akasema , “ kwa miaka minne” wakati analia, akisimama pale akisugua mikono yake. Na sehemu kubwa ya watu ikilia, wakimuangalia yeye, waluteri, wapresbiterian, na Nikasema “ kwa nini usiende madhabahuni na kupiga magoti chini” Akasemea hata hatua,

lakini alijua ameponywa. Kitu fulani kikachukua nafasi. Unaona? Alijua hilo: hakukua na kubashiri kokote kuhusu hilo ***(Waebrania 11:1***-2)

Nikasema , “Piga magoti chini” Na kwa mara ya kwanza kwa miaka minne, na magoti yote yaliyovunjika na sugu zote, zimefanyika (Zimefanywa) mfupa kuzunguka mfupa. Yule mwanamke kama msichana mdogo amejikunja kwenye magoti yake na machozi yakimchuruzika machoni mwake, akimwinulia mkono Mungu, kwanini umeyanyanyuliwa pale kirahisi, kama binti mdogo, amefunguliwa tu kwenye jukwaa ilikua ninini? Mungu atafanya njia kwaajili ya hilo. Sasa alituma madaktari, hiyo ni sawa. Na daktari ni wazuri na walifanya yote wangeweza kufanya, lakini Mungu alifanya njia. Hiyo ni sawa. Unaona? Baada ya daktari kushindwa kwa namna yake. Njia za Mungu ziko juu sana kuliko njia zetu
***(Isaya 55:8-9)*** Jambo la kustajabisha namna gani! [6].

Hapa ameketi ndugu Sidney Jackson , dada kutoka Afrika Kusini. Yeye anaweza kusimama hapa na kuchukua hilo somo na kuwaambia kiuhalisi kuhusu jambo fulani chini pale . Hakika watu wanaweza kuja kwenye sanamu na kupata kuponywa . Unaona,kwanini kwasababu?

Kama tu Dk Aegery alivyonifokea nje muda ule,kwa mimi kusema Shetani hawezi kuponya na akasema , “ Mtu anayesimama mbele ya wengi kama vile unavyofanya na thelojia mbovu namna hiyo kusema , “ kusema kwamba shetani hawezi kuponya” akasema “ Tuna mwanamke jirani yetu hushika kifuko kumzunguka. yeye na kuelekea pale na watukumzunguka na inatakiwa kudondosha pesa katika hiki kifuko; kasha atawasugua na kuchukua nyewele kutoka kichwani pake na damu kutoka mishipani mwao na kuiweka kwenye nywele na kuitipa nyuma yake na anakabiliwa kuangalia kuzunguka ugonjwa unarudi kwa watu” na kusema , “ Asilimia thelathini kati yao wanapata nafuu. Na halafu unasema shetani hawezi kuponya”.

Na ninafikiri “ oh jamani nikamwandikia na nikasema, “ mpendwa” nikasema, “inaniajabisha (ni kitu cha ajabu) kwangu kwamba mwamini wa chuo cha kilutheri angeweza kuitegemeza thelojia yake juu ya uzoefu badala ya neno la Mungu”. Unaona? “ Neno la Mungu linasema kwamba shetani hawezi kumtupa nje shetani ***(Mathayo 12:22-30)*** . Hiyo huuishi hapo. Yesu alisema hivyo, “ Nikasema, “ unaweza kushangaa kwanini watu wanaponywa kupitia hilo hilo uchawi ni kwasababu watu wenyewe wanafikiri kwamba wamemkaribia Mungu kupitia huo uchawi na uponyaji unaegemea kwenye imani, sio juu ya usahihi ulionao,jinsi gani ulivyo mzuri , jinsi gani nashika amri za Mungu au chochote kile inategemea kiukweli kabisa juu ya imani kwa neema yake na sifa yake. Na kwa jinsi vile

umekubali uponyaji na umeamini umeponywa na unaendelea ukiamini hilo namna hiyo, ataponywa kwa vile umeamini hilo na unaanza kushukuru hilo.

Na mchukue mtu ambaye ameketi hapa sio mgonjwa sana na hebu mwache aanze kulipata ndani ya moyo wake aamini yeye ni mgonjwa watamweka nje ya jingo. Jinsi imani yako ilivyo kwahiyo itakua hivyo kwako. Hiyo siyo sayansi ya mkristo. Simaanishi kuliakilo juu jambo. Lakini unaona,jambo la hilo ni ile hali unayoishi kwahiyo. [9].

Je yeye si wa ajabu? Sasa , wazia tunaamanisha kwamba kila kitu kinasalimishwa. " Mimi sio tena kile ninachowazia , wala siendelei kuwazia kama nilivyowaza, Bwana , ninaenda tu kuwazia kama wewe unavyowaza na umeniahidi nimeponywa ***(Isaya 53:4-5)*** Ninafikiri kwamba ninasalimisha mawazo yangu.Siendi tena kuwazia kuhusu ugonjwa wangu. Sitawazia kuhusu ugonjwa nilionao.Sitawazia chochote lakini nitawazia kile wewe umesema"

Sasa hapa mbele yenu amesimama mtu kama tu mlivyokuwa dakika chache zilizopita,ulikua unaumwa chini hapa, lakini kuna mtu mwenye afya amesimama pale. Yesu kristo anamuita mtu yule mwenye afya nyuma ya hilo.Sasa wewe tu kwa imani, kama alivyofunga macho yako,tembea kuendea ule mwili wenye afya halafu endelea tu kutembea endelea tu kuenda . [10].

Unaona, ni imani yako, kamwe sio hisi zako,kamwe sio namna lilivyo au kama mkono wangu haijanyooka….. Hilo halina jambo moja kufanya pamoja nalo.

Ni imani yangu ambayo hufanya hilo na halafu tunafanya hatua mpaka unapiga hatua kwa yule mtu na kutembea pamoja na hilo. Pale alipo. Hivyo ndivyo hufanya hilo.Imani yako, sio hisi zako, imani yako hufanya hilo. Lakini shukrani na sifa ziwe kwa Mungu. [12].

Nikasema kama tunatii njia iliyoandaliwa na Mungu ukoma utaondoka, ugonjwa utaondoka kila kitu kitaondoka, kila kitu kitaondoka, lakini tunapaswa kuja kwenye njia yake ya siku ya leo. Sasa kulowekwa Yordani hakutafanya chochote sasa,hilo lilikua kwaajili ya maana . Sheria ilikua kwa ajili ya wayahudi. Neema ni kwaajili ya Kristo. [12]

Wakati Mungu anapewa chochote,litakwenda kutukia, kwahiyo unapofikia vigezo vya Mungu,Kumbuka tu Mungu alijidhihirisha mwenywe na kulingalia yote yaliyobakia , wewe endelea tu kama kazi iliyokwisha malizika. Oh! Je hiyo si

ajabu? Oh, Jamani! Wazia mwambie Mungu tu, Mung alisema " wewe fanya hivi, na nitafanya hivi" vema, kama nitaenda kufanya hili, Yeye ataenda kufanya lile.

Sasa, shetani anasema " unaona, yeye anachelewa" Hiyo haifanyi tofauti yoyote. Wakati mmoja Daniel aliomba na siku ishirini na moja kabla malaika kumfikia yeye ***(Daniel 12:13)*** lakini alikatishwa tama, yeye alijua angekuja tu kwa vyovyote kwahiyo yeye alisubiri mpaka akafika pale. Hiyo ni oh! Hiyo n impale unapopata imani.

Lakini tunataka ibada za uponyaji wa roho kuponya ndani mle, kwasababu hiyo ndiyo inayoenda kudumu. Unapata uzima wa milele,uzima wa milele hautoweki wala kuzeeka,unadumu,unahaki vilevile. ***(Yohana 5:24).*** [13].

Hebu Roho Mtakatifu aje juu ya mtu yeyote hiyo ni kweli amepata kitu fulani chini pale. Uponyaji huja kutokea ndani hebu ule uponyaji uje kutoka ndani ya Roho ya yako ***(II Wakorintho 4:7).*** [14].

Natunaomba kwamba utalifanya hili kiuhalisi kwa kila mmoja wetu leo kwamba mioyo yetu nitachomwa, Roho zetu zitaponywa , nafsi zetu zitafanywa upya (2 wakorintho 5:17) ziumbwe kulingana na mtindo ambayo Mungu ametupa sisi. [15].

Kuna kitu kimoja nataka kua mwaminifu kwenu kuhusu hilo, Rafiki yangu. Njia ileile Mungu huponyea ipo juu ya msingi wa huduma kwake. Unaona? Kwenye msingi wa huduma kwake lazima tukubali uponyaji wetu kwenye msingi wa tutamtumikia yeye baada ya kuponywa.

Sasa, biblia ilisema " ungamaneni dhambi zenu mmoja kwa mwingine (Yakobo 5:16). Ombeaneni mmoja kwa mwingine, hivyo mnaweza kuponywa" unaona? Ipo kwenye msingi kwamba utamtumikia Mungu. Wengi wenu hapa labda, mpo katika hali ya kufa. Na lazima ufe kama kitu fulani hakitatokea . Basi nawataka ninyi mioyoni mwenu.

Sasa, tunaweza kukupanda mafuta (***Yakobo 5:14-15);*** tunaweza kukuombea , Mchungaji wako, na mimi, tunaomba maombi ya imani tukafanya kila kiitu tuwezacho. Lakini haitafanya nafuu yoyote mpaka utakapoingia wewe mwenyewe katika ushirika na kristo. Unaona? Unapaswa uje kwenye ushirika .[16]

Na haijalishi katika kila aina ya ibada neno lazima litangulie (Lipewe Kipaumbele). Lazima liwe la kwanza na uponyaji wa nafsi mara zote kwanza,

kwanini wakati mtu amezaliwa upya kwa Roho wa Mungu ***(Yohana 3:3-5)*** yeye ana umilele, uzima wa milele, na kamwe hawezi kutoweka. ***(Yohana 5:24)***

Lakini wakati mtu ameponywa kwa mwili wake, kwa ajili ya muda fulani tu. Lakini wokovu wa nafsi ni wa milele yeye anakua kiumbe kipya ndani ya Kristo ***(Wagalatia 6:14-15)*** wakati ameponywa nafsi yake. Lakini uponyaji wa kiungu umejumlishwa katika upatanisho kwa sababu upatanisho wa zamani ulikua mzuri mno kuliko wa zamani na upatanisho wa zamani ulikua na uponyaji . Na biblia inasema kwamba " Alichubuliwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa kwake sisi tuliponywa" Wakati uliopita tuliponywa ***(Isaya 53:4-5)*** oh! Ni la ajabu! [17]

Tunajua hatumponyi yeyote, lakini tunaomba tu kwa ajili yao. Na kamwe sijawahi kumponya hata mmoja bado lakini nina hakika ya kupata majibu makuu kwa maombi , kuona Mungu akiponya wagonjwa.

Na sio tu kwa uponyaji wa mwili , lakini uponyaji wa watu nafsi pia, ambao ni muhimu zaidi kuliko uponyaji wa mwili. Sasa aliwezekana kama utaishi maisha marefu kutosha utaumwa tena Biblia ilisema " Mateso ya mwenye haki ni mengi lakini Mungu humponya yeye kutoka katika yote hayo ***" (Zaburi 34:19)*** alivyo tuna ahadi ya mateso mengi , lakini ukombozi kutoka hayo. [18].

Na kwahiyo uponyaji wa kiungu,kitu kikungu,kitu kikuu ni uponyaji wa Kiungu wa nafsi, Mwili wa Kristo, unahitaji uponyaji kuliko kituo chochote ninachokijua, ni mwili wa kristo. Huo unavunjwa na theolojia za watu na tofauti za kidhehebu, mpaka unakua mwili mgonjwa na ninawaambia, unahitaji uponyaji mkuu kwahiyo ninaamini kwamba Bwana atafanya kitu kikubwa juu ya sehemu ya wake ambao uko pale. [19].

Sasa Bwana, ninakuomba wewe uwaponye, lakini kwa uponyaji wote mkuu! Kama utawaponya miili yao kutokana na kansa , kifua kikuu, kitu fulani,wataumwa ipo bado chini ya dhambi,laana,lakini hebu wao wapate uponyaji wa kiungu, uponyaji wa nafsi ambayo hufanya kiumbe kipya ***(2 Wakorintho 5:17)*** kupita hii maskani ya kale kwa ajili ya ukombozi wa mwili ***(Warumi 8:22-23)*** baada ya nafsi kukombolewa,ruzuku hili Bwana. [20]

Wakati tunakuja mwisho wa barabara , hatujui tu ni wapi na jinsi ambayo tungeenda kua wagonjwa. Tunaweza kuumwa kwenye akili zetu, inawezekana kua ni homa ambayo ningeweza kuzisumbua bongo zetu muhimu, na tunaweza kuongea chochote mwishoni mwa njia. Hatujui. Lakini, unaona kama tuliweka tayari nanga ndani ya Kristo, haidhuru ugonjwa gani ungetuchukua ama hali gani

tunayo wakati tunaenda, hiyo tayari imedumu. Tumepigwa mhuri mpaka siku ya ukombozi wetu. (**Waefeso 4:30)** inasema " Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa huyo mmetiwa mhuri mpaka siku ya ukombozi (sio ya kifo chetu)" unaona,baada ya kifo kupita, bado umewekwa muhuri. [21]

Daktasi alisema , " ndugu Branham, nimesema vitabu vyako juu ya uponyaji , kwa hakika ninakubaliana nawe, ninakwenda kukuambia, tuna mambo halisia hapa ninaweza kuyahakiki hayo kwa sayansi hebu mtu awe na kikuu au donda koo, au pumu, ama chochote ambacho ni hatari kabisa , tunajua kinaenda kumuua yeye, nitamuambia yeye hilo, kama yeye atapouza, kupunguka, hasira kukasirika na kuendelea mbele, yule mgonjwa angekufa tu. Haki kwa kawaida kama yule mgonjwa ni mkristo yeye hangeogopa kufa ni moja ya mambo tunapaswa kufanya kama kufa ni sehemu ya maisha, (kuishi) kwahiyo angeendelea mbele kuchukua hilo, nitaishi mpaka muda wangu utakapokwisha! Karibu ile tabia ingeacha tu lile jambo. Yeye angeendelea mbele na kuendelea kabla halijamuua yeye. [22]

Lakini kuna ugonjwa mkubwa kuliko ugonjwa wa kawaida na hiyo ni muhimu sana kwamba tungekua vizuri kwaajili ya tukio hili kuu ambalo linakaribia tu kutokea ni vizuri kua tayari. Ingekua bora kua mtu mgonjwa tayari pamoja na Bwana kuliko mtu mwenye afya asiye tayari kwenda na Bwana lakini hata hivyo , Mungu anatamani sana kwamba wote tuwe wazima na tayari nafsi na mwili (***Wathesalonike 5:23-24)*** kwa maana yeye hutusamehe maovu yetu yote na kutuponya magonjwa yetu yote. Amekufa kwa dhumuni maalumu (***Isaya 53:4-5)*** [23].

## NUKUU ZA KINGEREZA .

[1]. " Tazama" (63-0428) aya 4-9
[2] "Yesu Kristo ni Yeye yule jana na leo na hata milele (63-0627) aya 84-86
[3] " Yeye anajali, wewe unajali (63-0721) aya 43-44
[4] " Macho yao yalipofunguliwa (56-0420) aya E29-30
[5] Ishara ya Mbegu wakati wa mwisho (62-0319) aya E9
[6] Kufanya njia (56-0304) aya E25
[7] " Maswali na Majibu (64-0823M) COD uk 930-931
[8] " Maisha yaliyofikishwa na Kristo" ( 56-0213) aya E20 , E22-23
[9] "Isiyo ya kawaida (super natural) (56-0129) aya E 28
[10] " Nenda kamwamsha Yesu " 963-1130E) aya 274
[11] " Nitafanya nini kwa huyu Yesu " (63-1124m) aya 34
[12] " Njia iliyoandaliwa na Mungu kwa siku hii" (64-0206E) aya 12
[13] " Maono ya Patro (60-1204E) aya 95-97
[14] " Nguvu ya kubadili (65-120AE) aya 95-97
[15] " Umoja (62-0211) aya 10
[16] " Ng'ambo ya pazia la wakati (61-0305) aya 87-89
[17] " Msikilizeni yeye" (57-0125) aya E-11
[18] Ushirika (61-0410) aya E-2
[19] " Kristo aliyedhihirishwa kwa nyakati zote (64-0401) aya 1k
[20] " Mungu wa wakati muovu (65-0801m) aya 189
[21] " Ushuhuda wa ushahidi wa kweli (61-1105) aya 71
[22] " Njia ya kurudi (62-1123) aya E-93
[23]" Mshangao kuondoka kwa siri kwa kanisa (58-1012) aya E-5-E-6

---

Jiwe la kiroho la kujengea No. 19 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax(+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*